## Waziri Mkuu azindua NBC Kidigitali
UK2

kumekucha @kumekucha @kumekucha

mwanzo mpya

# KUMEKUCHA

Tovuti: wwwkumekucha.co.tz | ISSN 4562-9710 Toleo Na.37 Kumekucha Jumanne Machi 4, 2025 Bei Tsh. 1,000 | Ksh. 100

# Rais Dk. Samia mbeba maono aliyedhamiria kuipeleka Tanzania nchi ya asali na maziwa



> Uongozi wake umethibitisha kuwa CCM ni Chama kinachojali maslahi  ya wananchi

> Ameonesha uongozi bora haupimwi kwa jinsia, bali kwa maono, uchapakazi na utekelezaji wa ahadi kwa vitendo

UK8-9

## Yanga macho yotekwa Aziz KI ‘K’koo Derby’



UK 16



## Waislamu wapigwa marufuku kuswali swala ya Tarawehe

UK3

## Ulaya ina ubavu wa kuisaidia Ukraine  kijeshi ikiwa Marekani itakaa pembeni?

UK13



# Marufuku kuswali swala ya Tarawehe

Na Mwandishi Wetu

BARAZA Kuu la Waislamu katika Nchi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC)limetoa amri ya kusitishwa kwa swala ya Tarawehe kuswaliwa misikitini katika miji ya Mashariki mwa nchi hiyo kutokana na sababu za kiusalama.

Miji iliyokumbwa na marufuku ya kuswaliwa swala hiyo ni Goma, Bukavu, Uvira na Baraka ambayo hali ya usalama hairuhusu waislamu kutoka usiku kwenda msikitini kwenda kufanya ibada hiyo.

Tukio la kusitishwa kwa swala ya Tarawehe liliwahi kutokea mwanzoni mwa miaka 90 wakati wa vita vya ghuba kule nchini Iraq ambapo serikali ya nchi hiyo chini ya hayati Rais, Sadam Hussein ililazimika kuchukua uamuzi huo mgumu kwa sababu za kiusalama.

Swala ya Tarawehe ni miongoni mwa sunna ambazo huswaliwa katika mwezi wa Ramadhan tu baada ya swala ya Isha. Kwa mujibu Abu Hurairah (r.a) ameeleza kuwa Mtume wa Allah alikuwa akisisitiza swala ya usiku katika mwezi wa kufunga (Ramadhani), bila ya kuifaradhisha kwao.

Alikuwa akisema: Atakaye swali katika usiku wa mwezi wa kufunga, akiwa na imani na akitarajia malipo (kutoka kwa Allah (s.w),dhambi zake zilizotangulia husamehewa. (Muslim).

Marufuku ya Baraza hilo imetokana na hali ya usalama kuwa tete katika miji ya mashariki mwa nchi hiyo kutokana na vita inayoendelea kati ya majeshi ya serikali ya Congo DRC na waasi wa M23 ambao kwa sasa wanashikilia eneo kubwa la mashariki.

Taarifa ya Baraza hilo imeeleza hali ya usalama hairuhusu kutoka nje nyakati za usiku hivyo limewataka waislamu wote maeneo hayo kuchangangia swala ya Magharibi na Swala ya Isha na kurejea majumbani kabla ya giza kuingia.

Wakati hali ikiwa hivyo juhudi za kumaliza vita inayoendelea nchini zinaonekana kukatishwa tamaa baada serikali ya ya nchi hiyo kukataa kufanya mazungumzo ya maridhiano na waasi wa kundi la M23 ambalo limeteka maeneo makubwa mashariki mwa nchi katika miezi ya hivi karibuni.

Wiki iliyopita, serikali ya Uingereza ilitoa wito wa kuhusisha kundi la M23 katika "mazungumzo ya kujumuisha" kama sehemu ya juhudi za kupata suluhu ya kisiasa kwa mzozo huo.

Hata hivyo, katika mahojiano na BBC, Waziri Mkuu wa DR Congo, Judith Suminwa Tuluka, alisisitiza kuwa serikali yake inapendelea kuzungumza na Rwanda, nchi jirani ambayo inashutumiwa kwa kuunga mkono M23.

Kwa mujibu wa mamlaka za Congo, zaidi ya watu 8,500 wamepoteza maisha tangu mapigano yalipoongezeka mwanzoni mwa mwaka huu.Mamia ya maelfu wamelazimishwa kuondoka makwao wakihofia usalama wao wakati wa vita, ambapo wataalam wa Umoja wa Mataifa na wengine wakiangazia Rwanda kama nchi inayopiga jeki vita hivi.

'' Cha muhimu ni kwamba anayeleta vurugu na kutishia uhuru wa DRC ni Rwanda,'' Suminwa Tuluka anasema akinukuu ripoti kutoka kwa wataalam wa Umoja wa Mataifa mwaka jana ambayo ilitaja vikosi kati ya 3,000 na 4,000 vya Rwanda vilivuka katika mpaka wa Congo na vilisaidia wanamgambo wa M23.

Mazungumzo ya amani yaliyokuwa yakiongozwa na Angola mwaka jana mwezi Disemba yaligonga mwamba baada ya Rwanda kutaka serikali ya Congo izungumze moja kwa moja na waasi wa M23.

Waasi hao baadaye walionekana kuzidisha nguvu na kuteka baadhi ya miji mkuu kama vile Goma na Bukavu mwezi Januari na Februari.

Katika juhudi za pamoja za kutafuta suluhu zilizoanzishwa na mataifa ya Mashariki na Kusini mwa Afrika, viongozi wake walitoa wito wa kusitisha mapigano, na kuondoka kwa '' vikosi vya kijeshi vya kigeni ambavyo havikualikwa'' kutoka Congo na pia kutaka pande zote mbili kukaa pamoja kusuluhisha.. wakijumuisha M23''.

## Bodi ya Ithibati ya Waandishi wa Habari yapewa meno

Na Mwandishi Wetu,

BODI ya Ithibati ya Waandishi wa Habari, (Journalists Accreditation Board-JAB) imetakiwa kuhakikisha kuwa, waandishi wa habari wote nchini wanazingatia sheria, kanuni, viwango vya juu vya weledi, maadili, uwajibikaji, na miongozo inayosimamia taaluma ya uandishi wa habari.

Maelekezo hayo ni kati ya maagizo saba yaliyotolewa na Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Profesa Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi (MB), katika hotuba yake ya uzinduzi wa bodi hiyo uliofanyika tqrehe 03 Machi, 2025, katika Ukumbi wa Hotel ya Johari Rotana, jijini Dar es Salaam.

Profesa Kabudi amesema, Bodi ya Ithibati ya Waandishi wa Habari itasaidia kudhibiti uandishi usio wa kimaadili na kuongeza heshima ya taaluma hiyo, hivyo inatakiwa kuanza kwa kuwalea na kuwapa miongozo mbalimbali kuhusu taaluma yao.

Profesa Kabudi ameitaka pia Bodi hiyo kuhakikisha kuwa waandishi wa habari wanazingatia maadili ya taaluma kwa kutoa miongozo ya mafunzo ya mara kwa mara, na kuwa na utaratibu wa kushughulikia malalamiko na ukiukwaji wamaadili kwa haki na uwazi.

Agizo la pili kwa Bodi ni kuandaa na kusimamia utaratibu wa usajili wa waandishi wa habari kwa kuzingatia viwango vya kitaaluma, huku akisisitiza kuwa mfumo huo unatakiwa kua shirikishi na wenye kuendana na maendeleo ya teknolojia na mazingira ya sasa ya sekta ya habari.

Ameitaka JAB kuhakikisha inashirikiana na vyombo vya habari, vyuo vya mafunzo ya uandishi wa habari, na wadau wengine ili kuhakikisha waandishi wa habari wanapata mafunzo ya mara kwa mara na kuwa na ujuzi wa kisasa.

Profesa Kabudi ameiagiza Bodi kuandaa programu za uelimishaji ili kuongeza uelewa wa umma kuhusu umuhimu wa taaluma ya uandishi kusimamiwa ipasavyo.

Amesisitiza kuwa ni muhimu Bodi pia ikasaidia kuhakikisha kuwa waandishi wa habari wanatumia teknolojia kwa manufaa ya taaluma yao bila kuvunja maadili, katika ulimwengu wa sasa wa kidijitali, ikiwemo kudhibiti matumizi mabaya ya mitandao ya kijamii katika utoaji wa habari.

Kwa mujibu wa Profesa Kabudi Bodi inapaswa kushirikiana na mamlaka husika kuhakikisha kuwa waandishi wa habari wanafanya kazi zao kwa usalama bila vitisho, unyanyasaji, au vikwazo visivyo vya lazima, kwani Usalama wa wanahabari ni msingi wa uhuru wa vyombo vya habari.

Akitangaza kuzinduliwa rasmi kwa Bodi hiyo, Profesa Kabudi amesema, Serikali inatambua umuhimu wake, katika kuimarisha weledi, maadili, na uwajibikaji wa taaluma ya uandishi wa habari nchini, na kuahidi kuwa itaendelea kushirikiana nayo ili kuhakikisha taaluma ya habari inaimarika kwa manufaa ya taifa.

## Wizara ya madini,China wafanya majadiliano ya utafiti

Na Mwandishi Wetu

NAIBU Waziri wa Madini Dkt. Steven Kiruswa amekutana na Balozi wa Jamhuri ya Watu wa China nchini Chen Mingjian katika kikao kilichokenga kujadili fursa na maeneo mbalimbali ya ushirikiano katika Sekta ya Madini ikiwa ni mwendelezo wa mazungumzo kati ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Philip Mpango na kiongozi huyo .

Katika mazungumzo yao, Dkt. Mpango aliomba Serikali ya China kupitia balozi huyo kusaidia shughuli za utafiti wa madini Tanzania, ambapo baada ya mazungumzo yao, Serikali ya China imetuma wataalam wawili kutoka Taasisi ya Jiolojia na Utafiti ya Nchini humo ili kufuatilia na kujua mahitaji ya utafiti na maeneo mengine ya mashirikiano kati ya Tanzania na China.

''Kikao nilichokiongoza Machi 3 mwaka huu kimejadili maeneo ya ushirikiano, na sisi kwa upande wetu tumeweza kubaini maeneo matatu muhimu ambayo Serikali ya china inaweza kutusaidia katika shughuli za utafiti na kujenga uwezo wa watumishi wa Wizara kulingana na mahitaji,'' amesema Dkt. Kiruswa.

Maeneo matatu ambayo wataalam wa Wizara wakiongozwa na Dkt. Kiruswa waliyoweza kuyabaini ni pamoja na kusaidia upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kufanya utafiti wa kina wa jiofizikia (high resolution airborne geophysical survey) hususani kwa kuanzia eneo la Mkoa wa Dodoma;

Maeneo mengine ni pamoja na kusaidia upatikanaji wa fursa kwa ajili ya kuwajengea uwezo wataalam wa ndani katika maeneo ya teknolojia za kisasa kama vile ukusanyaji na uchakataji wa taarifa za jiosayansi; na kusaidia kuleta teknolojia za kisasa za utafiti na uchakataji wa taarifa za utafiti wa madini ikiwa ni pamoja na matumizi ya ndege nyuki katika utafiti wa madini nchini.

Wengine walioshiriki kikao hicho ni pamoja na Kamishna wa Madini Dkt. Abdulrahman Mwanga Kamishna, Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya Jilojia na Utafiti wa Madini Tanzania, (GST) Dkt. Mussa Budeba, Mkurugenzi wa Huduma za Jiolojia (GST) Dkt. Ronald Massawe, Afisa kutoka Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Bw. Makamba, Makamba na maafisa kutoka ubalozi wa China nchini Bw. Chu Kun na wataalm kutoka Taasisi ya Jiolojia China Bw. Ren Junping na Bw. Sun Kai.



## Makonda awaonya wanaopandisha bei mwezi wa Ramadhani

Na Mwandishi Wetu

MKUU wa Mkoa wa Arusha,Paul Christian Makonda ameonya wafanyabiashara wa Mkoa wa Arusha kujiepusha na upandishaji wa gharama za vyakula vinavyotumika zaidi wakati huu wa msimu wa mfungo wa Mwezi mtukufu wa Ramadhan, akitangaza kuja na Operesheni maalum ya kutembelea maduka ili kubaini wafanyabiashara wanaotumia mfungo wa Ramadhan kujitafutia faida ya ziada.

"Niwasihi, mwezi huu ( Mwezi mtukufu wa Ramadhan) sio mwezi wa kutengeneza faida, mwezi huu ni wa kutafuta baraka, faida unayoitafuta inaweza kuna kukugharimu sana, ukajikuta umepata magonjwa yakala mpaka na mtaji wako. Wenzako wanapofunga kwaajili ya kumuomba Mwenyezi Mungu, jitahidi na wewe uwe sehemu ya baraka ya kuhakikisha kuwa huwapi vikwazo." alisema Makonda.

Makonda pia kando ya kuarifu kuwa Mkoa unaandaa futari kwa ajili ya wananchi wa Mkoa wa Arusha, amewatakia Kheri pia Waislamu wa Mkoa wa Arusha kwenye mfungo waliouanza mwishoni mwa Juma lililopita sambamba na kwa Wakristo ambao wanatarajiwa kuanza mfungo wa Kwaresma hivi karibuni, akiomba kuwa funga zao zikafanyike kuwa baraka na kichocheo cha amani na Upendo katika Mkoa wa Arusha.

# Waziri Mkuu azindua NBC Kidigitali

Na Mwandishi Wetu

WAZIRI MKUU, Kassim Majaliwa amesema kuwa huduma jumuishi za kifedha ni kiungo muhimu cha ukuaji wa uchumi, kupunguza umasikini na kuchochea maendeleo ya jamii kwa ujumla.

Majaliwa ameyasema hayo jana alipozindua huduma mpya za kidijitali za Benki ya Taifa ya Biashara (NBC) katika ukumbi wa Super Dome, Masaki jijini Dar es Salaam.Alisema Serikali kwa kutambua hilo imedhamiria kuendelea kushirikiana na wadau wote ili kuhakikisha sekta ya kifedha inazidi kuwa jumuishi, fanisi, na yenye tija kwa maendeleo ya Taifa.

Aliongeza kuwa katika vipindi tofauti, Serikali imekuwa ikiandaa na kutekeleza mikakati ya Taifa ya kuboresha huduma jumuishi za kifedha."Mpango Mkakati wa Taifa wa Huduma Jumuishi za Fedha wa 2023 – 2028 ni mwendelezo wa mafanikio yaliyopatikana kupitia Mpango Mkakati wa Taifa wa Huduma Jumuishi za Fedha uliokamilika Desemba 2022"

Kadhalika,Majaliwa alisema,-jitihada nyingine ni kuandaa Mkakati wa Uchumi wa Kidijitali wa miaka 10 kuanzia mwaka 2024 hadi 2034. "Mkakati huu umeainisha malengo mahsusi ambayo kama nchi tunaazimia kuyatekeleza ili kufikia uchumi wa kidijitali."

Kwa upande wake, Naibu Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Sauda Msemo amesema sekta ya fedha imeendelea kuwa na ustahimilivu na hivyo kuwezesha shughuli mbalimbali za kiuchumi kufanyika.

Aidha, Naibu Gavana huyo ametoa wito kwa taasisi zote za kifedha zifuate viwango bora vya usalama wa mitandao na kuguundua haraka pale panapotokea udanganyifu wa aina yoyote.

Awali, Mkurugenzi Mtendaji wa NBC, Theobald Sabi alisema lengo la uzinduzi wa huduma hizo za NBC kidijitali ni kuboresha utoaji wa huduma za kifedha na kuzifanya zipatikane kwa urahisi. "Huduma hizo ni pamoja na ufunguaji wa akaunti, kuhamisha fedha, kupata mikopo bila ya kwenda katika tawi."

Pia, Kiongozi huyo alitumia fursa hiyo kuishukuru Serikali kwa kuhakikisha wananchi wengi wana namba za NIDA ambazo zinarahisisha ufanyaji wa biashara, utambuzi wa mtu na hivyo kumuwezesha kufungua akaunti."Namshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuboresha mazingira ya kiabiashara nchini."

## Jeshi la Zimamoto lachunguza moto maghala ya Ushirika

Na Mwandishi Wetu

JESHI la Zimamoto na Uokoaji mkoani Morogoro linaendelea kuchunguza chanzo cha moto ulioteketeza maghala ya Chama cha Ushirika wa Wakulima Morogoro (Mofacu), yanayotumiwa na Kampuni ya LMAX Limited kuhifadhi na kuchakata katani.

Moto huo ulizuka usiku wa kuamkia jana saa 6 usiku, karibu na kituo cha reli ya Kati katika Manispaa ya Morogoro.

Kaimu Kamanda wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Wilaya ya Morogoro, Mkaguzi Ramadhani Khalid, akizungumza leo Jumatatu Machi 3, 2025, amethibitisha tukio hilo na kusema juhudi za kudhibiti moto zilifanikiwa kwa kiasi kikubwa, huku uchunguzi wa chanzo cha moto ukiendelea.

"Tumefanikiwa kuudhibiti moto na kuokoa maghala matatu pamoja na ofisi za kampuni hiyo. Hata hivyo, uchunguzi wa kina utafanyika ili kubaini chanzo cha moto huu," amesema Khalid.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi wa Kampuni ya LMAX Limited, Evidius Rwegasira, moto huo umeharibu shehena kubwa ya katani pamoja na mitambo ya uchakataji, na kusababisha hasara inayokadiriwa kufikia zaidi ya Sh700 milioni.

# Chadema yavuna milioni 64 kampeni ya 'Tonetone'

Na Mwandishi Wetu

NAIBU Katibu Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Bara, Amani Golugwa, ametangaza kuwa kupitia kampeni ya Tone Tone, Watanzania wamechangia jumla ya Shilingi 64,315,150 tangu kampeni hiyo ilipozinduliwa.

Akizungumza na waandishi wa habari jana katika Makao Makuu ya CHADEMA, Mikocheni, Dar es Salaam, Golugwa amewashukuru Watanzania kwa imani yao na kujitokeza kwa wingi kuchangia chama kupitia njia mbalimbali.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, hadi kufikia Machi Mosi mwaka huu, fedha zilizokusanywa kupitia akaunti ya NMB zilifikia Shilingi 16,858,461, huku michango kupitia namba ya M-PESA (0744446969) ikifikia Shilingi 3,997,109. Pia, kupitia mfumo wa Kulipa Bili kwa M-PESA, chama kimepokea Shilingi 5,785,670, wakati njia ya Mix Bill kupitia mtandao wa Mix by Yas imekusanya Shilingi milioni 1.7.

Licha ya mafanikio haya, Golugwa ameeleza kuwa kumekuwa na changamoto katika baadhi ya mifumo ya kuchangia, hasa kwenye namba ya M-PESA, ambapo baadhi ya wachangiaji walipata ugumu kufanya malipo. Hata hivyo, amebainisha kuwa tayari chama kimewasiliana na mamlaka husika ili kurekebisha hitilafu hizo na kuhakikisha mfumo unafanya kazi kwa ufanisi.

"Nikiri kwamba zilitokea changamoto kadhaa katika mfumo wetu hasa kwenye namba hii ya 0744446969 na tumefanya mawasiliano na mamlaka husika na tupo katika kutatua changamoto hizo. Wachangiaji wengi wa Tone Tone walipata changamoto", ameeleza.

Kwa mujibu wa Golugwa, takwimu zinaonesha kuwa kuna kiwango kikubwa cha fedha ambacho kingeweza kuzidi Shilingi milioni 150 hadi 200, lakini mifumo ya malipo ilikuwa inawazuia baadhi ya wachangiaji. Amewahimiza Watanzania kuendelea kushiriki katika kampeni hiyo na kuhakikisha wanadondosha matone matone ili kufanikisha dhamira ya chama.

Katika jitihada za kurahisisha michango, Golugwa ametangaza kuwa sasa Watanzania wanaweza kuchangia kupitia programu tumizi ya Sim Banking ya CRDB kwa mfumo wa malipo ya kujirudia (subscription payments). Pia, M-PESA ya Vodacom imeruhusu malipo ya kujirudia kwa walio na akaunti zao. Hata hivyo, kwa mitandao mingine, bado mfumo huo haujawekwa.

# Ni kwa namna gani Upendeleo wa Kijinsia huwakwamisha Wanawake kushiriki katika Siasa Tanzania?

Na Maryam Nassoro

NILIINGIA katika siasa kwa sababu, niliona masuala mengi ya wanawake hayaingii kwenye sera mipango na bajeti kwa kuwa, nafasi nyingi za maamuzi zimeshikiliwa na wanaume.

“Hiyo ni kwasababu ya kushamiri kwa “Mifumo Dume” katika vyama vya Siasa nchini, nilitamani kuingia kwenye uongozi kufanya jambo la ziada kwa kuhakikisha masuala yanayohusu Wanawake na makundi mengine, yanaingia kwenye sera, mipango na bajeti, binafsi niliamini kila mwanamke ni kiongozi, anahitaji tu uthubutu na kuamua kushika hatamu.”

Hizo ni kauli za Lucy John Mtembo mwenye miaka 40 ni miongoni mwa Wanachama hai wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) na Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake wa Tanzania (UWT Mkoa wa Kaskazini Unguja).

Alianza harakati za siasa Miaka ya 2010, ambapo enzi hizo nafasi za uongozi kama Udiwani, Uwakilishi na Ubunge ulikuwa unashikiliwa na Wanaume wengi huku Wanawake wakionekana kuwa ni wapiga debe tu katika kampeni.

Anasema “Nimejifunza kuwa tunapaswa kuwa na uthubutu na utayari kujifunza mambo mapya na kujiwekea mipango inayotekelezeka ili tuwe viongozi wazuri.”Lucy anaeleza kuwa bado Wanawake wapo kidogo katika nafasi za uongozi na vyombo vya maamuzi.

Takwimu zinaonesha Zanzibar, hadi sasa kuna wanawake nane tu, waliowahi kugombania nafasi za uongozi majimboni, ambao walishinda uwakilishi, wanawake 18 walipata uwakilishi kupitia nafasi za viti maalum na hivyo, kufanya idadi ya wanawake katika Baraza la Wawakilishi kuwa 29 kati ya 77 waliyochaguliwa sawa na Asilimia 40.

Fatma Abdul Habib Ferej ni Katibu wa Ngome ya Wanawake wa Chama cha ACT Wazalendo, ambaye aliwahi kushika nafasi mbalimbali za uongozi katika Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, amesema bado wanawake wako kidogo katika nafasi za uongozi jambo ambalo linaji kuangaliwa.

Anna ameongeza kuwa Serikali inaendelea na jitihada katika kufikia malengo yaliyowekwa kupitia Dira ya 2050 na Mpango wa Maendeleo (ZADEP) 2021/2026 ambapo lengo katika nafasi za uongozi ni kufikia 50/50


Ripoti ya Sensa ya Watu na Makaazi ya Tanzania ya Mwaka 2022, inaonesha Zanzibar ina Wakaazi milioni 1.8 kati ya hao wanaume ni 915,492 na wanawake ni 974,281.hii ina maana kwamba wanawake ni Asilimia 51.6 ya Wakaazi wote wa Zanzibar, lakini wingi huo hauonekani katika nafasi za uongozi.

Chama cha Wandishi wa Habari Wanawake Tanzania Zanzibar (TAMWA ZNZ) ni Taasisi isiyo ya kiserikali, inayojishuhulisha na masuala ya utetezi wa haki za mtoto wa kike na kuhamasisha wanawake kushiriki katika nafasi za uongozi, Mkurugenzi Mtendaji wa TAMWA ZNZ, Dk. Mzuri Issa amesema vyama vingi vya siasa nchini, vimetawaliwa na mfumo dume jambo ambalo linawarudisha nyuma wanawake kugombea nafasi za uongozi.

Naibu Msajili wa vyama vya Siasa Tanzania, kwa upande wa Zanzibar Mohamed Ali Ahmed amesema kuongezwa kwa kifungu cha 10 C ndani ya Sheria ya Vyama vya Siasa nchini, kinatoa nafasi kwa wanawake kuongeza ushiriki wao.







# Haja ndogo inayokaa muda mrefu inaweza kuwa chanzo cha tezi dume

Na Mwandishi Wetu

KAMA chakula hai kinaweza kupunguza kasi ya ukuaji wa seli za saratani ya tezi dume, je kinaweza kushughulika na ukuaji wa seli za kawaida za tezi dume, BPH (benign prostatic hyperplasia)?

Sio kila kuvimba kwa tezi dume ni saratani, wakati mwingine inakuwa tu ni kuongezeka kwa ukubwa wa tezi lakini sio saratani, tunaiita BPH.Tezi dume imekalia shingo ya kibofu cha mkojo. Kama ikikua sana inaweza kuzuia mkojo usitoke. Kuzuia huku kunaweza kukasababisha mkojo kutoruka mbali au mkojo kuchelewa kutoka na kushindwa kutoa mkojo wote kwenye kibofu kiasi kwamba unakuwa unakojoa mara kwa mara.

Mkojo unaokaa muda mrefu kwenye kibofu unaweza ukawa chanzo cha maambukizi. Hali inazidi kuwa mbaya Zaidi pale tezi inapozidi kukua Zaidi.Njia zinazotumika siku hizi ni pamoja na suppliments pamoja na dawa.

Pia wanaweza kutumia njia ya upasuaji kama TUMT, TUNA na TURP. Ni majina yanayotokana na jinsi upasuaji unavyofanyika. Unapoona T kwenye hayo majina inamaanisha transurethral, ikiwa na maana wanaingiza mashine kupitia njia ya mkojo.

TUMT (transurethral microwave thermotherapy), daktari anaingiza kwenye uume kifaa kinachofanana na antenna na kuunguza huko ndani kwa microwaves. TUNA (transurethral needle ablation, huko ndani kwenye njia ya mkojo kunaunguzwa kwa sindano mbili za moto. Hizi njia mbili zinaitwa upasuaji ambao sio haribifu sana.

Njia ambayo huwa inatumika mara nyingi ni TURP, hapa daktari wa upasuaji anatumia waya kukata sehemu ya katikati ya tezi dume. Madhara ni pamoja na kujisikia vibaya baada ya upasuaji.

BPH imekuwa ikiwapata wanaume wengi kiasi kwamba madaktari wanadhani kuwa ni matokeo yasiyoepukika yanayokuja na umri kusonga. Lakini sio hivyo!

Kati ya miaka ya 1920 na 1930, kulikuwa na wagonjwa 80 tu katika ya watu wote China kwa miaka 15 linganisha na 80% ya wanaume wanaopata shida hii sasa hivi.

Utofauti huu ulitokana na chakula kikuu cha China na Japan kuwa ni cha asili kinanchotokana na mimea.

Unakumbuka utafiti uliofanyika na wanasayansi wa Pritin Foundation jinsi damu ya watu wanakula chakula hai ilivyoweza kupambana na seli za saratani ya tezi dume? Sasa walifanya tena kwenye seli za tezi dume ambayo imevimba japo sio saratani.

Ndani ya wiki mbili tu, wale waliokula chakula hai damu yao ilikuwa na uwezo wa kuzuia ukuaji wa seli za tezidume ambazo sio saratani pia. Matokeo hayakubadilika muda kadri muda ulipoendelea.. maana hadi miaka 28 baadaye bado ilikuwa na matokeo yale yale. Kwahiyo kama tukiendelea kula kiafya, seli za tezi dume zinaendelea kupungua na kubaki chini.

Baadhi ya mimea ina manufaa sana kwa tezi dume. Flaxseeds ipo juu ya orodha katika kutibu BPH. Kwenye utafiti wanaume walipewa vijiko 3 vya flaxseeds kila siku, matokeo yake yalikuwa mazuri sawa na kutumia dawa kama Flomax au proscar lakini bila madhara ya dawa kama kusikia kichwa chepesi na kushindwa kuhudumia ndoa.

. Je, inawezekana kuzuia BPH isitokee kabisa?

Kula kitunguu saumu na vitunguu maji vinasaidia kupunguza uwezekano wa kupata BPH. pia jamii ya kunde maharage, njegele, kunde, dengu pia ziasaidia kupunguza hatari ya kupata BPH.

Badala ya kufanyiwa upasuaji wa TVP (transurethral vaporization of prostate) huduma inayofanyika urology tumia TVP (textured vegetable protein) tunaiita nyama ya soya. Inafanya kazi vizuri Zaidi.

Vitu hivi ni vizuri na vitamu, fanya mazoezi jifunze jinsi ya kuandaa na kutumia kwenye chakula chako. Mfano, flaxseeds zinafaa sana kama mbadala wa mayai na unaweza ukatumia kwenye smoothie (juisi isiyochunjwa), kuongeza uzito wa mchuzi na katika mapishi mablimbali. Kama ni kwa ajili ya kinga, kijiko 1 kwa siku kinatosha kabisa. Unaweza ukazipata kwenye supermarkets

# Ni muhimu mnoo sasa Tanzania kuingia vitani kuilinda DRC



Na Mwandishi Wetu

AMA kwa hiari (kupenda) au kwa lazima (shuruti) ni wakati muafaka sasa kwa majeshi ya Tanzania kuingia moja kwa moja uwanja wa vita (Full scale) huko DRC ili kurejesha amani na kuwafutilia mbali waasi wa M23. Sababu za kufanya hivyo zipo na kwa uchache sana nitaziweka hapa.

1. DRC ni jirani muhimu wa Tanzania akiwa mdau mkubwa zaidii wa Tanzania kibiashara kupitia bandari ya Dar. Hivyo kuzorota kwa amani ya DRC ni kuzorota kwa biashara ya bandari hapa Tz.

2. DRC ni mwanachama kamili wa jumuiya ya Africa mashariki, jumuiya ambayo kuwepo kwake kumechangiwa na juhudi za Tanzania huku jumuiya ikiwa na mikataba inayotamka kila mwanachama kusaidiwa kulindwa dhidi ya adui yoyote anayevamia au kuteteresha amani ya nchi mwanachama. Ni muda wa vitendo sasa.

3. Kwa kuwa hakuna mgongano wowote wa kimaslahi kama Tanzania itaingia kuisaidia DRC (Mpaka sasa hakuna nchi yoyote iliyokiri kuwasaidia waasi wa M23 (Japokuwa sote tunajua Rwanda ndio mhusika mkuu) na wakati huo huo Tanzania hatufungamani na waasi wa M23), hivyo uwanja upo wazi.

4. Historia ya Tanzania kujiingiza kwenye mizozo ya namna hii na kufanikiwa iko wazi. (Tanzania ilifanya hivyo 2013 huko huko DRC kwa kufurusha hao M23, na ilifanya pia hivyo kule kwenye visiwa vya Comoro).

5. Tayari askari kadhaa wa Tanzania wanaolinda amani huko DRC wanaripotiwa kutekwa na kuuawa na waasi wa M23 katika kipindi hichi cha uchukuaji wa mji wa Goma. Tuna sababu ya kuchukua hatua!

6. Utawala wa DRC tangu kuondolewa kwa dikteta Mobutu mwaka 1997 mpaka leo hii umekuwa ni utawala rafiki na ndugu katika nyanja zote muhimu za kiserikali. Kama Tanzania itaamua kukaa kimya wakati huu DRC ikiteketea basi hakutakuwa tena na maana ya kuendeleza undugu na urafiki na DRC. Utakuwa ni unafiki kwa 100%.



# Asili ndo itumike kuweka usawa wa kijinsia

Na Mwandishi Wetu

MIPAKA ya kijinsia bado ipo kwenye jamii zetu. Na mbaya zaidi wanawake Bado wanazingatiwa kama watu wa makundi maalumu.Mwanamke kuzingatiwa kama mtu wa kundi maalumu ndilo jambo linaloendeleza uwepo wa mipaka ya kijinsia katika fursa mbalimbali za kijamii ikiwemo fursa ya uongozi.

Ukianzia kwenye ngazi ya shule watoto wa kike mara nyingi wanapatiwa misaada ya kujisitili na mambo mengine kuliko watoto wa kiume kwahyo hizo hali zinaendelea kuwafanya wanawake waonekane kwamba wao ni wa makundi maalumu hivyo wanahitaji zaidi uangalizi wa wanaume na taifa kwa ujumla.

Usawa hautakiwi kuwa wa upendeleo bali kila binadamu anayetakiwa kuwa sawa na binadamu mwenzake basi awe sawa kiasili. Asili ndo itumike kuweka usawa lakini ikiwa kila siku tutaimba kuhusu kulazimisha fursa Kwa wanawake basi tutakuwa tunaendelea kuwafanya wanawake waonekane wao ni watu dhaifu kiasili.

Ili kuondoa changamoto zote zinazominya ushiriki wa wanawake kwenye masuala mbalimbali ya kijamii tuhakikishe tunaondoa misingi yote inayowaweka wanawake kwenye makundi maalumu na nafasi za upendeleo.Hakuna haja ya kulazimisha mada bali kila jambo liwe kiasili na mabadiliko yaanzie kwenye familia zetu.

Hakuna namna mwanamke anaweza kuwa na nguvu kama mabadiliko hayataanzia kwenye familia yake.Wanawake kama wanataka kuwa kama wanaume na wawe sawa kwenye mambo yote ya kijamii na kitaifa basi waache unyonge na wasiwe wanapenda penda misaada na kuonekana kama wao ni kama watu wa makundi maalumu. Je wataweza?? Kazi kwao.

Uwezo kiakili na utendaji wa shughuli mbalimbali, wanawake wamekuwa wakionesha ufanisi mdogo sana na wengi wao wamekuwa wakiamini na kuwategemea wanaume katika kufanikisha shughuli hizo.Wanawake wenyewe wanawaamini sana wanaume kuliko wanavyojiamini wao wenyewe kwenye mambo mbalimbali yanayotegemea nguvu na akili.



# Rais Dk. Samia mbeba maono aliyedhamiria kuipeleka Tanzania nchi ya asali na maziwa



Na Mwandishi Wetu

RAIS Samia Suluhu Hassan ni kiongozi wa kipekee ambaye amebeba matumaini makubwa ya Watanzania. Utendaji kazi wake umejikita katika kuimarisha uchumi, kuleta maendeleo, na kuhakikisha mshikamano wa kitaifa.

Kama mwanamke wa kwanza kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ameonesha kuwa uongozi bora haupimwi kwa jinsia, bali kwa maono, uchapa kazi wake na utekelezaji wa ahadi kwa vitendo.

Katika kipindi chake cha miaka 4, Rais Samia amesimamia kukamilika na uendelezaji wa miradi mikubwa kama Reli ya Kisasa (SGR), Bwawa la Umeme la Julius Nyerere ,Uwekezaji mkubwa Bandari ya Dar es salaam.

Uwanja wa Ndege wa Msalato, Daraja la Kigongo Busisi, na Upanuzi wa Huduma za Maji Safi na Umeme Mijini na Vijijini. Ameboresha sekta za afya na elimu kwa kujenga Shule na Hospitali, kuongeza upatikanaji wa vifaa tiba, na kuboresha maisha ya Wafanyakazi.

Jitihada zake za kuvutia wawekezaji zimeimarisha Uchumi wa Taifa na kupanua fursa za ajira kwa Watanzania walio wengi.Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, aliwahi kusema. Mwalimu Nyerere alitambua uwezo wa wanawake katika kuleta mabadiliko. Kauli yake imejidhihirisha kupitia uongozi wa Rais Samia, ambaye amekuwa mfano bora wa utekelezaji wa maono hayo kwa vitendo.

Rais Samia mara kwa mara amesisitiza kuwa wanawake si wanyonge. aliwahi kusema. Kupitia hotuba zake na vitendo vyake, amewahamasisha wanawake kote nchini kushiriki kikamilifu katika maendeleo. Pia ameongeza uwakilishi wa wanawake kwenye nafasi za uongozi serikalini na taasisi mbalimbali.

Uongozi wake umethibitisha kuwa CCM ni Chama kinachojali maslahi ya wananchi. Miradi inayotekelezwa ambayo imegusa maisha ya watu wa kawaida ni udhihirisho wa dhamira ya Chama ya kuleta maendeleo jumuishi. Rais Samia ameimarisha imani ya Watanzania kwa CCM kupitia uwajibikaji na utekelezaji wa ahadi za Chama.

Rais Samia ni mfano bora wa uongozi thabiti unaothamini mshikamano, maendeleo, na uwajibikaji. Ameonyesha kuwa wanawake ni nguzo muhimu ya maendeleo ya Taifa. Kwa utendaji wake wa bidii na maono amekuwa turufu ya CCM kwa Watanzania na kielelezo cha matumaini kuelekea uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba 2025.

CCM kwa aina ya Mgombea waliomteua haina shaka kuwa itashinda kwa kishindo na kuweka historia nyingine kwa kuwa na Mgombea Mwanamama wa Kwanza aliyeshinda Urais kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi kuliko vipindi vingine vyote vya uongozi katika historia ya Tanzania.



# Milima ya Udzungwa na sifa ya kipekee duniani

NA VICTOR MAKINDA

UTALII ni kitendo cha mtu au kundi la watu kutoka eneo moja kwenda eneo jingine kwa lengo la kujionea kumbukumbu za kihistoria au vivutio vya aina nyingine kama vile wanyama, misitu, mito mikubwa, bahari majengo au inaweza kuwa kitu kingine chochote kama vile maeneo ilipopiganwa vita, maeneo waliyozaliwa watu maarufu ama viongozi wa dini.

Utalii una umuhimu mkubwa katika ustawi wa maisha ya binadamu. Pamoja na kuwa ni kiburudisho cha akili lakini pia utalii unaongeza ufahamu kuhusu mazingira na vitu mbali mbali Mwenyezi Mungu alivyovumba ambavyo vinavyoipamba Dunia yetu nzuri.

Hifadhi ya Milima ya Udzungwa, inayopatikana katika mikoa Morogoro na Iringa ni moja ya eneo lenye mvuto wa kipekee wa kitalii. Hifadhi hii ya Milima ya Udzungwa ni nyumbani kwa aina nyingi za wanyama, mimea,aina tofauti toauti za ndege na viumbe vingine ikiwa ni pamoja na maporomoo makubwa ya maji yanayojulikana kama maporomoko ya maji ya Sanje.

Utajiri wa Maliasili za hifadhi hii ni mkubwa. Ni eneo lililotuzwa vizuri na lenye uoto wa asili unaovutia, jambo ambalo linaipa akili ya mtembeleaji/mtalii wa hifadhi hii uwezo wa kujifunza na kujionea utajiri mkubwa wa maliasilia ambazo Mungu ametujalia sisi Watanzania.

Kuelezea uzuri wa Hifadhi ya Milima ya Udzungwa kunahitaji kurasa nyingi zaidi. Kama nilivyokwisha kusema awali, Hifadhi ya Milima ya Udzungwa ina aina nyingi za mimea viumbe na wanyama.

Katika kundi la wanyama linalojulikana kwa lugha ya kimombo kama Big Five, ikiwa inawajumuisha, Simba, Tembo, Kifaru, Twiga na Chui, mnyama mmoja tu ambaye ni Kifaru ndiye hapatini hifadhini hapo.

UPEKEE WA HIFADHI YA MILIMA YA UDZUNGWA

Hifadhi ya Taifa ya Milima ya Udzungwa yenye vilele vingi kikiwemo kilele kirefu zaidi katika hifadhi ya milima hiyo, kilele cha Ruhomero chenye urefu wa mita 2576, ina aina 2500 za mimea huku ikiwa na maporomoko mengi ya maji yakiongozwa na maporomoko marefu zaidi kuliko yaliyopo Hifadhi zote za Taifa, maporoko ya maji ya Sanje yajulkanayo kama Sanje Water Fall.

Maporomoko hayo yana urefu wa mita 1978. Maporomoko mengine ya maji katika Hifadhi hiyo ni Prince Bernard, Njokamoni. Ndani ya Hifadhi hii ya Milima ya Udzungwa kuna mapango makubwa yaliyobeba historia ya biashara ya utumwa na vita uliyopiganwa kati ya wahehe na Wajerumani.

Licha ya mapango hayo kubeba historia ya biashara ya utumwa ni mahali muhimu kwa ibada za jadi. Mapango maarufu yanayopatikana katika Hifadhi hiyo ni Mwanaburele, Mwanihana, Nyumba Nitu, Mdene.

Hifadhi ya Taifa ya Milima ya Udzungwa ina mengi mazuri yenye kuvutia ambapo orodha yake ni ndefu. Kuna aina nyingi za mijusi, akiwemo mjusi pekee anayepatikana katika hifadhi hii na hapatikani mahali pengine Duniani. Mjusi huyu maarufu anayejulikana kwa jina la Udzungwa Rizard ni miongoni mwa vivutio vikubwa vya watalii katika hifadhi hiyo.

Umaarufu wa hifadhi ya Udzungwa ni pamoja kuwa ni hifadhi yenye aina nyingi za ndege kuliko hifadhi yoyote barani Afrika huku ikiwa na aina 400 za ndege.

Kati ya aina hizo 400 zinazopatikana katika hifadhi hiyo, aina mbili za ndege zinapatikana katika hifadhi hiyo tu na huwezi kuwaona ndege hao mahali pengine duniani.

Moja ya aina ya ndege hao ambao anatajwa kuwa ndege mkongwe kabisa Duniani ni kwale wa mistari, ambapo watafiti wanamtaja kuwa aliishi miaka Milioni 40 iliyopita.Aina hiyo ya kwale ipo hatarini kutoweka ambapo juhudi kubwa zinapaswa kuelekezwa katika kumuhifadhi ndege huyo adimu na adhimu.

Pia kuna ndege anayejulikana kama Chozi Mbawa Nyekundu au Sunbed, ambaye naye huwezi kimuona mahali pengine duniani.Hakika Hifadhi ya Udzungwa ni kisima cha utalii na mvuto wa kimazingira huku ikiwa kuna aina nyingi za nyoka katika hifadhi hiyo.

Katika Hifadhi ya milima ya Udzungwa pamegunduliwa aina mpya ya nyoka ikiwemo Duniani, aliyevumbuliwa na kuonekana kwa mara ya kwanza katika hifadhi hiyo hivi karibuni.

Nyoka huyo anayepewa jina la Matilda s horned Viper alibainika mwaka 2009 na kuthibitishwa kuwa ni aina mpya ya nyoka Duniani mwaka 2011.

Pia ndani ya hifadhi hii kunapatikana aina ya kinyonga wa kipekee anayejulikana kama Bearded Pigmy Chamillion ambaye ni mfupi na rangi yake hubadilika taratibu tofauti na aina nyinginze za vinyonga. Sambamba na hilo, kuna kuna aina 1200 za vipepeo kati ya aina hizo, aina tatu zinapatika katika Hifadhi ya Milima hii tu na huwezi kuipata mahali pengine Duniani.

KUHUSU MAPOROMOKO YA SANJE.

Maporomoko ya Sanje ndani ya milima ya udzungwa ni eneo lenye utajiri mkubwa na kivutio kisicho kifani. Maporomoko hayo ndiyo nembo ya hifadhi hiyo,

Ukiwa njiani kwenda kwenye maporomoko hayo unakutana na madhari nzuri ya misitu minene ya kitropiki yenye hali ya hewa nzuri yenye kuburudisha nafsi.

Katika maporomoko haya maarufu ya Sanje unaweza kuona aina kumi na moja za wanyama aina ya nyani wanaopatikana katika hifadhi ya Udzungwa, huku aina mbili tu za wanyama hao unaweza kuiona katika hifadhi hiyo tu na si mahali pengine Duniani.

Aina hizo ni mbega wanaojulikana kama Ngorago au Sanje Crested Mangabay, na Mbega mwekundu,anayejulikana kama Iringa red Collubus Monkay. Nyani aina ya Ngoraga amefanyiwa uzoeshaji wa kitabia na biniadamu (Habituation) ambapo mnyama huyo hamUogopi biniadamu na mtalii anaweza kumsogela kwa karibu kabisa na hata kucheza naye.

Katika maporomoko hayo maarufu ya Sanje, kuna bwawa kubwa la asili mahali maji yanapotua, ambapo mtalii anaweza kuogelea pasipo madhara yeyote.

Kileleni mwa maporomoko hayo, mtalii anapata fursa ya kutazama kwa upana mkubwa madhari ya bonde la Kilombero, hususani mashamba ya miwa ya Kilombero huku akiburudika na hali ya hewa nzuri sambamba na sauti za ndege na maji yanayoporoka.

Mandhari nzuri ya maporomoko hayo yanatoa fursa kwa mtalii kupiga picha katika uwanda mpana.Yapo maeneo mazuri na salama ya kuweka kambi na kufanya hafla na sherehe ndogo ndogo (picnic) sambamba na kujifunza masuala ya uhifadhi.

FAIDA ZA KUTEMBELEA HIFADHI ZA MILIMA YA UDZUNGWA

Hifadhi ya Milima ya Udzungwa ni mahali salama kwa afya ya mwili na akili kwa mtalii yeyote anayeitembelea. Hifadhi hii ni Hifadhi ya kutembea kwa miguu huku usalama ukiwa umeirishwa kwa asilimia mia moja kujikinga na wanyama wakali.

Mtalii katika Hifadhi hii ana nafasi ya kuona kila anachokitaka kwa ukaribu zaidi kwani hii ni hifadhi ambayo mtalii anatembea kwa miguu.

Usalama ni asilimia mia moja kwa kuwa mtalii haruhusiwi kupanda milima peke yake pasipo askari wa wanyama pori na muongozaji wa watalii.

Hifadhi hii ni mahali pazuri pa kuimarisha afya ya mwili kwani licha ya watu wengi wa mijini kuzoea usafiri wa vyombo vya moto, ndani ya hifadhi ya Udzungwa ni mahali sahihi pa kunyoosha viungo na misuli kwani mtalii atatembea kwa miguu kwa umbali atakaona unamfaa.



# Kunyamaza katika Uislamu ni hekima kubwa

Na Mwandishi Wetu

KATIKA Uislamu, kunyamaza ni kipengele muhimu cha maadili na tabia nzuri. Mtume Muhammad (SAW) alihimiza umma wake kuzingatia maneno yao na kuchagua wakati sahihi wa kuzungumza.

Hii ni kwa sababu maneno yanaweza kuwa na athari kubwa kwa watu wengine, na matendo ya mtu yanaweza kuathiriwa moja kwa moja na maneno hayo.Kwanza, Uislamu unafundisha kwamba kunyamaza kunaweza kusaidia katika kuzuia migogoro na mizozo. Maneno yasiyofikiriwa yanaweza kusababisha kutoelewana na hata uhasama kati ya watu. Katika Hadithi, Mtume Muhammad (SAW) alisema:

“Yeyote anayeamini kwa Allah na Siku ya Mwisho, na aseme jambo la kheri au anyamaze.”

Hii inasisitiza umuhimu wa kuzungumza kwa hekima na busara, na kunyamaza inapobidi.

Pili, kunyamaza kunaweza kusaidia katika kutafakari na kufanya ibada kwa unyenyekevu. Waislamu wanahimizwa kutumia muda wao katika kutafakari juu ya maajabu ya uumbaji wa Allah, kusoma Qur’an, na kutafakari juu ya maana ya maisha. Kunyamaza kunatoa nafasi ya kujitathmini na kuimarisha imani.

Mtume (SAW) alijulikana kwa muda wake wa kunyamaza na kutafakari, akionyesha mfano wa jinsi kunyamaza kunavyoweza kusaidia katika kujikurubisha kwa Allah. Tatu, kunyamaza kunaweza kusaidia katika kudhibiti hasira na hisia mbaya. Wakati mtu anapokasirika, kuna uwezekano mkubwa wa kusema maneno ya kuumiza ambayo yanaweza kuwa na athari mbaya kwa mahusiano ya kijamii na familia.

Kwa kunyamaza, mtu anaweza kupunguza madhara ya haraka ya hasira na kuepuka kufanya mambo yanayoweza kujuta baadaye. Qur’an inasema, “Na waabudu Rahmani (Mwenye kurehemu) ni wale wanaotembea kwa unyenyekevu duniani, na wanapohutubiwa na wajinga, husema: Salama.” (Qur’an 25:63).

Aidha, kunyamaza ni muhimu katika kusikiliza vizuri. Kusikiliza ni sehemu muhimu ya mawasiliano bora, na kunyamaza kunampa mtu nafasi ya kumsikiliza mwenzake kwa makini.

Hii inasaidia katika kujenga uelewa mzuri na uhusiano wa kina na wengine. Mtume Muhammad (SAW) alifundisha umma wake umuhimu wa kusikiliza kwa makini na kutafakari kabla ya kujibu.

Kwa kumaliza, kunyamaza ni tabia inayothaminiwa sana katika Uislamu. Inasaidia katika kujenga amani, kutafakari, kudhibiti hisia, na kuboresha mawasiliano.

Kwa kufuata mfano wa Mtume Muhammad (SAW) na mafundisho ya Qur’an, Waislamu wanaweza kuimarisha maisha yao ya kiroho na kijamii kwa kujua ni lini waongee na lini wanyamaze.



# Dakika 10 za majibizano kati ya Trump- na Zelensky katika Ikulu ya Marekani

Rais wa Ukraine alikuwa na matumaini chanya ya kuondoka katika Ikulu ya White House Ijumaa baada ya mazungumzo chanya na Donald Trump, ambayo yangekamilika kwa kusainiwa kwa makubaliano ya madini ambayo yangeipatia Marekani umiliki katika mustakabali wa Ukraine, ingawa si hakikisho la usalama kamili kwa Ukraine.

Badala yake, Volodymyr Zelensky alikabiliwa na manemo makali mbele ya vyombo vya habari vya kimataifa, baada ya Rais Trump na Makamu wake Rais JD Vance kudai shukrani zaidi kwa msaada ambao Marekani imetoa kwa miaka mingi.

Rais wa Ukraine alijibu mapendekezo kutoka kwa washirika wake hao wenye nguvu zaidi kwamba anapaswa kufanya juhudi zaidi ili kukubaliana na Vladimir Putin kuhusu kusitisha mapigano. Walimjibu kwamba alikuwa "akidhihaki".

Zelensky alielekezwa hatimaye kuondoka Ikulu ya White House mapema kabla yeye na Trump hata kufanya mkutano wa waandishi wa habari kama ilivyoratibiwa.Na mkataba wa madini, ambao ulikuwa ukitangazwa na kupigiwa upatu na pande zote mbili wiki hii, haukusainiwa.

"Rudi wakati utakapokuwa tayari kwa ajili ya mchakato wa amani," Trump aliandika kwenye mtandao wa kijamii kabla ya gari la Zelensky kuondoka.Kulikuwa na maeneo kadhaa ya mivutano mikubwa katika mkutano huo.

Hapa tunaangazia maeneo manne;

1) Hasira zawapanda Zelensky na Vance

Katika nusu saa ya mazungumzo ya amani na taratibu mwanzoni, mvutano ulianza kuzidi katika Ofisi ya rais wakati Vance aliposema "njia ya amani na ya mafanikio ni kushiriki katika mchakato wa kidiplomasia".

"Hicho ndicho anachofanya Rais Trump," alisema.Zelensky aliingilia kati, akirejelea uchokozi wa Urusi katika miaka ya kabla ya uvamizi wake rasmi miaka mitatu iliyopita ikiwa ni pamoja na kushindikana kwa usitishwaji mapigano 2019."Hakuna aliyemzuia," alisema akimaanisha rais wa Urusi Vladimir Putin.

"Diplomasia gani hiyo JD unayoizungumzia? Unasemaje?" Alisema.Majibizano hayo yakawa ya wasiwasi, na Vance akajibu: "aina ambayo itamaliza uharibifu kwa nchi yako."Makamu huyo wa rais alimshutumu Zelensky kwa kukosa heshima na "kudai" hivyo mbele ya vyombo vya habari vya Marekani.

Ilikuwa ni utetezi wa Vance juu ya mbinu ya Trump ya kumaliza vita - kwa kuanzisha mazungumzo na Putin na kushinikiza kusitishwa kwa haraka kwa mapigano - ambayo awali ilizidisha mvutano na kiongozi huyo wa Ukraine.

2) 'Usitueleze tutajisikiaje'

Baada ya Vance kumkosoa rais wa Ukraine kuhusu changamoto za jeshi lake, Zelensky alijibu: "Wakati wa vita, kila mtu ana matatizo, hata wewe. Lakini una fursa nzuri lakini huioni sasa utaihisi katika siku zijazo."

Maoni hayo yalimpa nafasi Trump kuingilia na kumleta kwenye majibizano ambay hadi wakati huo yalikuwa kati ya Zelensky na makamu wa rais.Hapa alikuwa kiongozi wa Ukraine akieleza Trump ameshindwa kufahamu hatari ya kimaadili ya kushirikiana na mwanzilishi wa vita.

Ujumbe wa Zelensky ulikata kiini cha kile ambacho wakosoaji wanasema ni makosa ya kimsingi ya Trump katika kushughulika na Urusi.Kwamba kwa kuikingia kifua Moscow iliyotengwa na kutafuta usitishaji vita haraka anahatarisha kumtia moyo Putin, kudhoofisha Ulaya na kuiacha Ukraine katika hatari.

Trump amekuwa akiashiria kwamba vita ni aina ya mzozo kati ya pande mbili ambazo zinapaswa kuwajibika kwa lawama na chanzo chake.Lakini Zelensky alikuwa akijaribu kuonya juu ya matokeo mabaya ya mtazamo huu.Kiongozi wa Ukraine akamwambia Trump moja kwa moja katika Ofisi ya rais: Ifurahishe Urusi, na vita vitakuja kwako.

Kauli iliyoamsha hasira ya Trump ;"Usituambie tutajisikiaje.Huna uwezo wa kutuambia hivyo," alisema, sauti yake ikiongezeka."Huna nafasi sasa hivi," alimwambia. "Unacheza kamari na maisha ya milioni ya watu."Majibizano haya yanaweza kumpa sifa Zelensky miongoni mwa wale waliotaka kumuona akimpinga Trump; lakini wakati huu pia unaweza kuamua mustakabali wa vita na amani ya Ulaya.

3)'Haujawahi kuwa peke yako'- Trump

Katika moja ya hatua za mazungumzo hayo, Zelensky alisema: "Tangu mwanzo wa vita, tumekuwa peke yetu na tunashukuru."Hii ilimkasirisha Trump, ambaye mara kwa mara ameelezea vita hivyo kama mzigo kwa walipa kodi wa Marekani.

"Haujawahi kuwa peke yako," alisema. "Haujawahi kuwa peke yako. Tulikupa $350bn kupitia rais huyu mpumbavu - ," akimrejelea Biden.Kisha Vance akamuuliza Zelensky ikiwa alikumbuka kushukuru Marekani wakati wa mkutano na kumtuhumu kwa kufanyia kampeni upinzani yaani Democrats kipindi cha uchaguzi mkuu wa Marekani mwaka jana.





# Je Ulaya ina ubavu wa kuisaidia Ukraine kijeshi ikiwa Marekani itakaa pembeni?

MARA baada ya Rais wa Ukraine Volodymyr Zelensky kufukuzwa Ikulu ya Marekani kufuatia malumbano yake na Rais Donald Trump na Makamu wa Rais JD Vance, viongozi wa Ulaya walituma jumbe nyingi kumuhakikishia kwamba watasimama nae hadi dakika ya mwisho

Siku iliyofuata tu Jumamosi (1 Machi), Zelensky alitua Uingereza, akaonana na Waziri Mkuu wa nchi hiyo Kier Starmer na hata kufanya mazungumzo na Mfalme Charles. Siku ya Jumapili akakutana na viongozi wengine wa Ulaya waliokutana London kujadili mustakabali wa usalama wa bara lao.

Pamoja na maonyesho yote haya, swali kubwa ni; Ulaya ina ubavu wa kuisaidia Ukraine kijeshi ikiwa Marekani itakaa pembeni?

Kuna vitu vingi Ulaya inahitaji kuweka sawa, muda ni mchache na haina utashi wa kisiasa wa kutosha.Ukianza na bajeti ya kijeshi tu, kwa mujibu wa International Institute of Strategic Studies, bajeti ya kijeshi ya Urusi kama nchi ni kubwa kuliko ile ya bara zima la Ulaya. Wakati Urusi imetenga 6.7% ya pato lake la taifa, wakati Ulaya (wanachama wa Nato ukiondoa Marekani) wanatumia wastani wa 1.6%.

Ili kukabiliana na Urusi, wataalamu wanasema Ulaya itapaswa kuongeza matumizi yake ya kijeshi hadi kufikia wastani wa 3.5% ya pato la taifa la umoja huo, hasa kwa nchi za Mashariki ya Ulaya zilizo karibu na Urusi kama vile.Tayari tunaona nchi kadhaa za Ulaya zimeanza kuongeza bajeti yao ya kijeshi. Uingereza kwamfano, siku chache zilizopita imetangaza mpango wa kukata pesa inayotuma kwa misaada nje ya nchi na kuielekeza katika bajeti yake ya ulinzi.

Idadi ya wanajeshi na uongozi kwenye uwanja wa vita

Ukraine inakiri zaidi ya wanajeshi wake 40,000 wameuawa katika kipindi cha miaka mitatu ya Vita vya sasa vya Ukraine. Kuhusu wanajeshi walio tayari kupigana, wakati Urusi ina wanajeshi takribani 250,000 walio tayari kupelekwa Ukraine muda wowote, Ulaya haiwezi kutoa wanajeshi 150,000, ambao Zelensky anasema watahitajika kulinda amani na kumzuia Putin asivamie tena.

Viongozi wengi wa Ulaya wamesema wakijitahidi sana, basi wanaweza kupeleka wanajeshi wasiozidi elfu thelathini (30,000). Ulaya inakabiliwa na ukosefu wa kiongozi mmoja (mtu au ofisi) wa kijeshi. Kwa ujumla Ulaya (wanachama wa Nato) ina wanajeshi wapatao 1.47 ambao wako tayari kupigana, lakini hawana komandi moja ya kuwakusanya na kuwaongoza. Kwasasa Nato inategemea hii kazi kufanywa na Marekani. Hivyo Marekani akikaa pembeni, Ulaya itakuwa na kazi ya kutafuta kiongozi ambaye anaweza kuvikusanya, kuvijumuisha na kuviongoza vikosi vya nchi zote za Ulaya wanachama wa Nato kuwa kikosi kimoja chenye nguvu, badala ya kila nchi Kwenda kukabiliana na Urusi kama nchi moja moja.

Ulaya ina teknolojia ya kutosha, lakini inahitaji uwekezaji mkubwa kuanza kutengeneza vifaa vikubwa na bora zaidi - hasa vya masafa marefu kama ambavyo Marekani imetoa kwa Ukraine ndani ya miaka hii mitatu

Silaha za anga na utashi wa kisiasa

Moja ya ndege za kijeshi za Marekani zilizoko nchini Ukraine, A CV-22B Osprey

Nchi za Ulaya pia zinategemea vifaa vya anga vya Marekani na uwezo wake mkubwa wa kukusanya intelijensia, uwezo ambao Ulaya haina.

Hata katika usafirishaji wa silaha, Ulaya imekuwa ikitegemea sana miundombinu na uratibu wa Marekani kufanikisha kusafirisha msaada wa vifaa uliopeleka Ukraine. Wakati Nato inavamia Libya mwaka 2011, hata kama Ulaya ndio ilikuwa inaongoza mapambapo, walitegema zaidi vituo vya mafuta vya Marekani kujaza vifaa vyao.



# Je, nchi za Kiarabu zina mpango gani wa kuijenga Gaza?

Misri na nchi kadhaa za Kiarabu zinafanyia kazi mipango ya kuijenga upya Gaza, kuhakikisha Wapalestina wanasalia katika eneo hilo bila ya kuhama na kuanzisha utawala mpya katika Ukanda huo bila ya kuwashirikisha Hamas.

Mipango hiyo ni kujibu mapendekezo ya Rais wa Marekani Donald Trump ya kuwahamishia Wagaza na kuwapeleka Misri, Jordan na nchi nyingine, pamoja na kuchukua udhibiti wa Gaza, na kuigeuza kuwa kile alichokiita "eneo la mapumziko la Mashariki ya Kati."

Shirika la habari la Reuters limeripoti kuwa mapendekezo manne yameandaliwa kuhusu Gaza, lakini pendekezo la Misri kwa sasa linaonekana kuwa ndio msingi wa juhudi za nchi za Kiarabu ili kutoa njia mbadala kwa mpango wa Trump.

Kulingana na vyanzo vya BBC, Cairo inakaribia kukamilisha mpango huo, unaohusisha kusafisha vifusi, kujenga upya Gaza, kuamua jinsi Wapalestina watakavyo ishi katika kipindi hiki na utaratibu wa utawala baada ya vita. Hata hivyo, mustakabali wa makundi yenye silaha huko Gaza, hususan Hamas na Islamic Jihad, bado unajadiliwa.

Misri inasema mpango huo utaandaliwa kwa ushirikiano na utawala wa Marekani. Vyanzo kutoka Misri pia vimeiambia BBC, Umoja wa Mataifa (UN) na Umoja wa Ulaya (EU) watashiriki katika mpango huo. Misri inashauriana na nchi za Kiarabu, zikiwemo Jordan na Saudi Arabia, kuhusu mpango huo kuelekea mkutano wa kikanda mjini Riyadh tarehe 21 Februari, ambao unaweza kujumuisha pia ushiriki wa Mamlaka ya Palestina.

Chanzo hicho kimeongeza kuwa mpango wa Misri unalenga zaidi katika kujenga upya Gaza na kuugawa Ukanda huo katika maeneo matatu, kila eneo likiwa na kambi kubwa 20 kwa ajili ya wakazi kuishi, na kutoa mahitaji ya kimsingi kama maji na umeme.

Kulingana na mpango huo, maelfu ya nyumba ndogo ndogo na mahema vitapelekwa katika maeneo salama kwa makazi kwa muda wa miezi sita, sambamba na kuondolewa kwa vifusi.

Mpango huo pia utasisitiza ulazima wa kuruhusu mafuta na vifaa vya ujenzi kuingia Gaza.

Kulingana na mpango wa Misri, ujenzi mpya utafadhiliwa na wafadhili wa nchi za Kiarabu na kimataifa, na karibu makampuni 50 ya kimataifa yaliyobobea katika ujenzi yatajenga makazi ndani ya miezi 18 katika maeneo matatu yaliyopendekezwa ya Gaza.

Na ufadhili huo utasimamiwa na kamati inayojumuisha wawakilishi wa nchi za Kiarabu na kimataifa.Pendekezo hilo pia linajumuisha kuundwa kwa eneo salama na kizuizi cha kuzuia uchimbaji wa mahandaki kwenye mpaka wa Gaza na Misri.

Hata hivyo, siku ya Jumamosi Waziri Mkuu wa Israel Benjamin Netanyahu alitangaza, hataruhusu nyumba ndogo ndogo na vifaa vya ujenzi kuingia katika Ukanda wa Gaza, akitaja wasiwasi wa usalama licha ya kwamba hiki ni kifungu cha makubaliano ya hivi karibuni ya kusitisha mapigano.

Chanzo hicho kinaeleza, pendekezo moja katika mpango wa Cairo linahusisha makundi hayo kupokonywa silaha mara tu taifa la Palestina litakapotangazwa ndani ya mipaka iliyokuwepo kabla ya Vita vya Siku Sita.

Jerusalem Mashariki itakuwa mji mkuu wa taifa hilo na kutakuwa na eneo salama - eneo ambalo bado halijaamuliwa - ili kuihakikishia Israeli kwamba hakuna vitisho vitatoka Gaza.


Pendekezo hilo pia linahusisha kuunda kamati ya Wapalestina itakayosimamia Gaza bila ya ushiriki Hamas. Majeshi ya nchi za Kiarabu na kimataifa yataisaidia kwa muda kamati hiyo katika kusimamia Ukanda wa Gaza.

Hamas hapo awali ilieleza kuwa iko tayari kuachia utawala wa Gaza kwa kamati ya kitaifa lakini ilitaka kuwa na jukumu la kuchagua wanachama wake na haitokubali kutumwa kwa vikosi vyovyote vya ardhini bila ya ridhaa yake.

Vipi kuhusu mpango wa Trump?

Rais wa Marekani amerudia kueleza mpango wake wa kuwahamisha Wapalestina kutoka Gaza, ili kuibadilisha ardhi hiyo kuwa eneo la uwekezaji wa kitalii na kwa manufaa ya Wapalestina wenyewe kwa vile hawataishi tena kwenye vifusi. Trump alitishia kusitisha misaada kwa Misri na Jordan ikiwa hazitawachukua Wapalestina.

Baada ya mkutano wa hivi karibuni mjini Washington kati ya Trump na Mfalme Abdullah II wa Jordan, msemaji wa rais wa Marekani, Caroline Levitt, alisema Mfalme Abdullah amemweleza wazi Trump kwamba anapendelea Wapalestina wabaki Gaza wakati wa mchakato wa ujenzi. Lakini Trump, bado anapendelea kuwahamisha Wapalestina kutoka Gaza.





# Patcho Mwamba unataka nini?

KADRI siku zinavo zidi kwenda Mkurugenzi wa Band ya FM Academia Patcho Mwamba Kipenkwila anazidi kuongeza Wanamuziki ndani ya FM.Na safari hii ni upande wa marapa baada ya Mirinda Nyeusi aka Colonell Nangaa pia amemuongeza kundini rapa mwingine aliyekua band ya Malaika ya Christian Bella Heritier Pembele.

Ujio wa rapa huyo ndani ya Fm Academia ni kama mwiba mchungu kwa rapa mwingine G 7 hali ya mnyukano wa maneno ulitokea jukwaani katika onyesho lao pale Kitambaa Cheupe Tabata Alhamis ya Jana wakati show inaendelea. Wimbo ya Heshima kwa Wanawake ukiwa hewani ambapo ki uhalisia marapa walioghani ni G 7 ..Toto Kalala na Papy Catalog Chuck Noriss..

Wakati uo jukwaani alikuwepo G 7 ..Mirinda Nyeusi Colonel Nangaa na Heritier Pembele .. tukio la ajabu ni pale G 7 kukataa kuwaachia wenzake vipande ambavyo yeye hakuimba ..shida ilikuja kilipo fika kipande kiliicho imbwa na Papy Catalog cha bata kutingisha body la nyuma

G 7 baada ya kumaliza kipande chake Heritier alianza ku rap kipande hicho cha bata kutingisha body la nyuma ghafla G 7 akafanya ishara ya kukata muziki na kuongea maneno ya hovyo

Ndipo Mkurugenz Patcho Mwamba aliekua pembeni ya jukwaa kusimama na kuamrisha sebene hilo liendee

Nilimuuliza pembeni Heritier shida nini akasema G 7 hapendi wenzake wafanye hizo rap bali anataka afanye yeye mwenyewe pekee zote zilizopo katika tungo hiyo.Ndio mana nauliza Patcho Mwamba unataka nini ..maana nia yako ni nzuri kuboresha kikosi chako lakin kuna baadhi ya watendaji wanabania wenzao ..



KUMEKUCHA
MICHEZO
JUMANNE,MACHI 4, 2025

# Yanga macho yote kwa Aziz KI 'K'koo Derby'



NA MWANDISHI WETU

MASHABIKI wa Yanga kama ilivyo kwa wenzao wa Simba wanachotamani ni kuona timu yao inashinda tu dhidi ya Simba na siyo vingine, lakini kazi hiyo licha ya kufanywa na wachezaji mbalimbali ndani ya kikosi cha Wananchi hao, lakini macho mengi zaidi yameelekezwa kwa 'Bwana harusi' Aziz Ki.

Staa huyo ndani ya kikosi cha Yanga hivi karibuni alidumu midomoni mwa mashabiki na wapenda burudani kwa ujumla, pale alipofunga ndoa ya kifahari na msanii maarufu Tanzania Hamisa Mobeto.

Muda mfupi baada ya kufanyika tukio hilo lililokusanya idadi kubwa ya mastaa Jijini Dar, mashabiki wa timu hiyo na hata wapinzani wao walianzisha minong'ono wakidai huenda kiwango cha mwamba huyo uwanjani kinaweza kupungua kutokana na matumizi ya ndoa yaliyomkabili kwa zaidi ya wiki nzima.

Lakini tofauti na matazamio hayo mwamba huyo akawa ndiyo kama amezidisha moto, kwani alikuwa akipachika mabao na kutoa asisti katika mechi mbalimbali zilizofuata na kuisaidia timu yeke kudumu kileleni katika msimamo wa Ligi Kuu ikifikisha Pointi 58.

Uimara huo ndiyo uliomfanya awe tegemeo la kikosi hicho katika mechi hiyo muhimu ijayo Jumamosi hii itakayowakutanisha dhidi ya Simba, ambapo furaha ya mashabiki wa Wanajangwano hao ni kumuona Aziz Ki akianza kukitumikia kikosi cha kwanza.

Mechi hiyo imeanza kuteka simulizi kwa asilimia kubwa katika miji mbalimbali na hasa vijiwe vya mijini vinavyokutanisha mashabiki wa Simba na Yanga.

# Arajiga, Kayoko wapigwa msasa VAR

Na Mwandishi Wetu

WAAMUZI 20 wakiwamo maarufu kama Ahmed Arajiga, Herry Sasii, Ramadhani Kayoko na Tatu Malogo, wameanza mafunzo maalum ya teknolojia ya usaidizi kwa waamuzi (VAR).

Kozi hiyo yenye lengo la kuboresha ufanisi wa waamuzi hao inafanyika kwa muda wa siku tano katika ukumbi wa Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam kuanzia leo Jumatatu hadi Ijumaa ya wiki hii chini ya mkufunzi wa VAR kutoka FIFA, Tameer Dorry.



Kwa mujibu wa orodha iliyotolewa na TFF, washiriki katika kozi hiyo ni Ahmed Aragija, Amina Kyando, Herry Sasii, Tatu Malogo, Nasir Siyah, Mohamed Simba, Ramadhan Kayoko, Alex Pangars, Abdallah Mwinyimkuu, Esther Adabert, Frank Komba, Kassim Seif na Ally Ramadhan.

Wengine ni Hamdani Said, Mohamed Mkono, Janeth Balama, Glory Tesha, Zawadi Yussuph, Siraji Mkwaju na Shaban Mussa.

